

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS

SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Kumb. Na. JA.9/18/01"A"/60

07/11/2024

TANGAZO LA KUITWA KAZINI

Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma anapenda kuwataarifu waombaji kazi kwa nafasi ya Dereva waliofanya usaili tarehe **24/07/2024** kuwa matokeo ya waombaji kazi waliofaulu usaili huo ni kama yalivyoorodheshwa katika tangazo hili.

Muombaji aliefaulu usaili anatakiwa kuchukua barua za kupangiwa kituo cha kazi katika Ofisi za Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma –Ofisi ya Zanzibar zilizopo katika Jengo la **KATIBA NA SHERIA** Mazizini Zanzibar–Gorofa ya tatu ndani ya siku saba kutoka tarehe ya tangazo hili na baada ya hapo barua hiyo itatumwa kupitia anuani yako ya Posta.

Aidha, Muombaji kazi aliefaulu usaili na kupangiwa kituo cha kazi anatakiwa kuripoti kwa Mwajiri katika muda ambao umeainishwa kwenye barua ya kupangiwa kituo cha kazi akiwa na vyeti halisi (**Originals Certificates**) vya kumalizia masomo kuanzia kidato cha nne na kuendelea ili vihakikiwe na mwajiri kabla ya kupewa barua ya Ajira. Kwa yule ambae jina lake halipo katika tangazo hili atambue kuwa hakupata nafasi/hakufaulu usaili, hivyo asisite kuomba kwa mara nyingine nafasi za kazi zitakapotangazwa.

MUHIMU:

Unapokuja kuchukua barua za kupangiwa kituo cha kazi, Unapaswa kuwa na kitambulisho kwa ajili ya utambuzi; Vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na:- Kitambulisho cha Uraia, Hati ya kusafiria, Kitambulisho cha Mkazi, Kitambulisho cha Mpiga kura au Kitambulisho cha kazi, Leseni ya Udereva **AU** Barua kutoka kwa Sheha wa Shehia unayoishi /Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa/Kijiji unachoishi.

NA	MAMLAKA YA AJIRA	KADA	MAJINA YA WALIOITWA KAZINI
1	Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA)	Dereva Daraja La II	1. Othman Hamisi Juma

LIMETOLEWA NA;

**KATIBU
SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**